

VIONGOZI WA KANDA YA MASHARIKI WAASWA KUTUMIA FURSA WALIZONAZO KUIMARISHA SEKTA YA KILIMO NCHINI

WAZIRI Mkuu Mstaafu mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda amewataka viongozi wa Mikoa na Halmashauri zinazounda Kanda ya Mashariki kutumia fursa za bandari, barabara, reli, viwanda, nguvu kazi na hali ya hewa nzuri walizonazo kuiimarisha kiuchumi kanda hiyo kwa kulima, kuchakata na kusafirisha bidhaa na mazao mbalimbali kama vile ufuta, mchele, Karafuu, chikichi na miwa ili kuweza kufikia lengo la Serikali la kuwa na chakula toshelevu kwa mahitaji ya ndani na nje ya nchi.



Mheshimiwa Pinda ameyasema hayo jana tarehe 01.08.2023 katika uwanja wa JK Nyerere, Morogoro wakati alipokuwa akifungua rasmi maeondesho ya Nane Nane Kanda ya Mashariki inayoundwa na mikoa ya Morogoro, Tanga, Dar-Es-Salaam na Pwani na kusisitiza kwamba azma ya Serikali ni kuhakikisha ifikapo mwaka 2030 kilimo kiweze kuchangia asilimia kumi zaidi kwenye pato la Taifa.

“Licha ya kwamba kilimo kinamchango mkubwa kwenye pato la Taifa letu bado kinatutesa kwa sababu ya changamoto za umaskini, elimu na maradhi lakini tunamshukuru Rais Samia kwa kuendelea kuimarisha sekta za elimu na afya nchini jambo ambali litapelekea tondokane na changamoto hizo na kuwa na nguvukazi ya kutosha zaidi katika shughuli za kilimo na hatimaye kufikia malengo ya Taifa ya kuimarisha sekta ya kilimo nchini” alieleza Pinda.



Vilevile Mheshimiwa Pinda amewaasa viongozi wa Halmashauri zinazounda Kanda ya Mashariki kuhakikisha wanaandaa na kutenga ardhi ya kutosha kwa ajili ya vijana na wasiache kuwashirikisha wanawawake na vijana katika shughuli za kilimo kama Kauli Mbiu ya Mwaka huu inavyosema kwamba "Vijana na Wanawake ni Msingi Imara wa Mifumo Endelevu ya Chakula" kwani mwanamke akielewa kuhusu chakula bora taifa linaweza kuondokana na tatizo la udumavu na vijana wakishirikishwa vizuri sekta ya kilimo itaimarika zaidi kwa sababu wao ndilo kundi kubwa tena lenye wasomi wengi na nguvu pia.



"Serikali imeanzisha program ya Kujenga Kesho Iliyo Bora (BBT) kwa vijana ambapo vijana wanapatiwa mafunzo ya kilimo na wanapohitimu kila kijana anapewa shamba ili aweze kuendesha shughuli za kilimo na hii yote ni kuhakikisha vijana wetu tunaanza kuwajenga sasa hivi. Kwa sasa program hii inatekelezwa katika mkoa wa Dodoma, hivyo itakapowafikia katika Kanda yenu, mashamba yawepo tayari kwa ajili ya kuwagawia wahitimu. Anzeni sasa Kuandaa mashamba hayo." Alisisitiza Pinda.



Kwa upande mwingine, Msheshimiwa Pinda amewataka viongozi wa Halmashauri zote kutanguliza maslahi ya wananchi na kuwatumikia kwa moyo, kuwa waadilifu na kuwa mfano bora wa maadili mema kwao huku wakiendelea kutunza mazingira na vyanzo vya maji kwa kupanda miti kwa wingi ili kuendelea kuimarisha hali ya Hewa.



Aidha Msheshimiwa Pinda amesema Serikali inaendelea kuimarisha sekta ya kilimo kwa kuweka ruzuku kwenye mbolea na kuongeza uzalishaji wa mbegu bora huku ikikazia upatikanaji wa viwatilifu, upimaji wa afya ya udongo, kuongeza matumizi ya matrekta badala ya jembe la mkono, kuimarisha huduma za ugani na tafiti za kilimo. Hivyo amewataka viongozi wa Serikali za Mitaa kuhakikisha wanaunga mkono juhudi hizo za Serikali kwa kusimamia vizuri fedha zinazoletwa na Serikali kwenye maeneo yao ili ziweze kufanya yale yaliyokusudiwa.

MWISHO